## Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Bioanuwai, Misitu, Nyanda za Miti, na Maeneo Chepechepe Katika Delta na Bonde la Rufiji

# Ripoti ya Warsha Ya Washikadau Ihusuyo Mpango wa Uendeshaji wa Mazingira Wilayani Rufiji Iliyofanyika Utete Rufiji 29 – 30 Juni 2000

**Imetayirishwa na Karanja F. & Hogan R.**



**Technical report No. 15**

**Septemba 2000**

**Kwa mambo zaidi wasiliana na**

Meneja wa Mradi
Mradi wa Usimamizi Mazingira Rufiji
P O Box 13513
Dar es Salaam, Tanzania.
Tel: 44 Utete Rufiji or 2666088 / 0741 322366 Dar es Salaam
Email: rempute1@bushmail.net or iucndar@epiq.or.tz

---

[1]The Rufiji District Council implements Rufiji Environment Management Project with technical assistance from IUCN – The World Conservation Union, and funding from the Royal Netherlands Embassy.

# Rufiji Environment Management Project - REMP

**Project Goal:** To promote the long-term conservation through 'wise use' of the lower Rufiji forests, woodlands and wetlands, such that biodiversity is conserved, critical ecological functions are maintained, renewable natural resources are used sustainably and the livelihoods of the area's inhabitants are secured and enhanced**.**

**Objectives**

- To promote the integration of environmental conservation and sustainable development through environmental planning within the Rufiji Delta and Floodplain.
- To promote the sustainable use of natural resources and enhance the livelihoods of local communities by implementing sustainable pilot development activities based on wise use principles.
- To promote awareness of the values of forests, woodlands and wetlands and the importance of wise use at village, district, regional and central government levels, and to influence national policies on natural resource management.

**Project Area**

The project area is within Rufiji District in the ecosystems affected by the flooding of the river (floodplain and delta), downstream of the Selous Game Reserve and also including several upland forests of special importance.

**Project Implementation**

The project is run from the district Headquarters in Utete by the Rufiji District Administration through a district Environmental Management Team coordinated by the District Executive Director. The Project Manager is employed by the project and two Technical Advisers are employed by IUCN.

Project partners, particularly NEMC, the Coast Region, RUBADA, The Royal Netherlands Embassy and the Ministry of Natural Resources and Tourism, collaborate formally through their participation in the Project Steering Committee and also informally.

**Project Outputs**

At the end of the first five –year phase (1998-2003) of the project the expected outputs are:

An Environmental Management Plan: an integrated plan for the management of the ecosystems (forests, woodlands and wetlands) and natural resources of the project area that has been tested and revised so that it can be assured of success - especially through development hand-in-hand with the District council and the people of Rufiji.

Village (or community) Natural Resource Management Plans: These will be produced in pilot villages to facilitate village planning for natural resource management. The project will support the implementation of these plans by researching the legislation, providing training and some support for zoning, mapping and gazettement of reserves.

Established Wise Use Activities: These will consist of the successful sustainable development activities that are being tried and tested with pilot village and communities and are shown to be sustainable

Key forests will be conserved: Forests in Rufiji District that have shown high levels of plant biodiversity, endemism or other valuable biodiversity characteristics will be conserved by gazettement, forest management for conservation, and /or awareness-raising with their traditional owners.

# Yaliyomo

**Yaliyomo** ... **3**

**1 Historia ya Warsha** ... **4**

**2 Ufunguzi** ... **5**

**3 Utaratibu Mwingine wa Maendeleo ya Mipango ya Menejimenti ya Maliasili** ... **9**

**4 Uchambuzi wa Washikadau** ... **12**

4.1 Vikundi vitumiavyo Maliasili vya ndani ... 12

**5 Majadiliano ya Vikundi** ... **14**

5.1 Kikundi cha Kilimo ... 14
5.2 Kikundi cha Wanyama Pori ... 15
5.3 Kikundi cha Rasilimali ya Misitu ... 16
5.4 Kikundi cha Rasilimali za Uvuvi ... 18

**6 Mapendekezo kwa Chaguo za Menejimenti Kuhusu Masuala Yaliyotolewa Kupitia Kwenye Mijadala Ya Vikundi** ... **20**

**7 Hitimisho** ... **28**

**8 Tathmini ya Warsha** ... **29**

**9 Waliohudhuria** ... **31**

**10 Wajumbe wa Vikundi** ... **33**

# 1 Historia ya Warsha

**Bw. Francis Karanja- Afisa Programu**

Wilaya ya Rufiji katika Pwani ya Kati ya Tanzania ni eneo kubwa lenye msitu wa mikoko katika pwani ya Mashariki ya Afrika. Mikoko hii inachangia sehemu kubwa ya uvuvi wa maji kupwa na kujaa, inatoa maeneo ya mazalio muhimu Kitaifa kwa Kamba, na ina umuhimu wa kutosha katika eneo lake na kimkoa. Wilaya ya Rufiji pia ina maeneo mengine mengi ya misitu na maeneo ya miti – ambayo mengi ya hayo yametokana na mafuriko toka Mto Rufiji ambao unatoa maji ya juu na kati kwa misitu kando ya bahari, misitu ya kinamasi, maeneo yenye miti isiyo na manufaa vichaka na maeneo chepechepe juu na kando ya uwanda wake wa mafuriko. Zaidi ya watu 150,000 wanaishi katika delta za mto Rufiji na uwanda wake wa mafuriko wengi wao wakiishi kwa kutegemea uvuvi , kilimo na uvunaji wa misitu, miti, na mauzo ya sehemu ya majimaji. Kuna misitu ya pwani kavu yenye thamani sana wilayani Rufiji katika nyanda za juu mbali na delta na uwanda wa mafuriko ambayo kwa hakika ina mimea anuwai yenye umuhimu katika eneo hilo, kitaifa na huenda kimataifa – kama vile msitu wa Milima ya Kichi na Hifadhi za Misitu ya Nyamuete – Namakutwa, na Mchungu.

Katika mwongo uliopita, misitu, maeneo ya miti maeneo chepechepe ya Rufiji yamekuwa katika shinikizo linaloongezeka kutokana na sababu nyingi, ikiwa ni pamoja na ongezeko la idadi ya watu, mavuno yasiyokuwa endelevu ya mbao na samaki, mabadiliko ya maeneo ya mikoko kuwa ya kilimo na matumizi ya msitu wa kando ya mto na maeneo ya miti kwa kuni. Katika kipindi cha nyuma kulitolewa pendekezo la kuendeleza kilimo shadidi kidogo cha kamba, ambacho kingetishia ukamilifu wa mfumo wa ikolojia wa misitu ya mikoko. Mikoko, tambarare ya mafuriko na maeneo ya maji safi pia vinatishiwa na maendeleo wilayani kama vile uboreshaji wa mfumo wa barabara, likiwemo na daraja katika mto Rufiji. Shughuli za utafutaji wa madini, na pia shughuli za maendeleo za sehemu za juu za mito zinazojumuisha ujenzi wa mabwawa ya mitambo ya umeme na mpango wa uchimbaji wa visima. Uingiliaji kati wa menejimenti kukabiliana na shinikizo hizi umekwamishwa na ukosefu wa taarifa za ikolojia na uchumi wa kijamii, ushirikishaji wa washikadau usiotosheleza, data zisizotosheleza kuhusu kiwango na kipimo cha mabadiliko ya matumizi ya ardhi, na uwezo usiotosheleza wa uhusiano wa upangaji na menejimenti ya muda mrefu katika kiwango cha wilaya. Katika hali hii ndipo Umoja wa Hifadhi Duniani ikishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji na washikadau wengine katika viwango vya mkoa na kitaifa ilipoanzisha mradi huu wa awamu ya kwanza wa mradi wa menejimenti ya Mazingira wa Rufiji. Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji inatekeleza mradi huu kwa msaada wa kiufundi toka Umoja wa Hifadhi Duniani. Serikali ya Uholanzi inatoa msaada wa kifedha.

Lengo la Mradi wa Menejimenti ya Mazingira ya Rufiji ni kukuza mpango wa uhifadhi wa muda mrefu kwa utumiaji wa busara wa misitu ya Mto Rufiji ya chini, maeneo ya miti na maeneo chepechepe,ili baioanuwai iwe inahifadhiwa, shughuli nyeti za ikolojia zinadumishwa, maliasili zinazoweza kuanzishwa upya na kuwa endelevu kwa manufaa na uchumi wa wakazi unapata hifadhi na kuendelezwa. Mawili kati ya malengo makuu na shughulli za awamu hii ya mradi yanalenga kwenye hatua za kuendeleza na utaratibu wa maendeleo na kutekeleza mpango wa menejimenti ya Mazingira. Hatua hizi ni:

1. Kuanzisha misingi wa kuleta uwiano kati ya malengo ya hifadhi na mahitaji ya maendeleo ya binadamu, kwa kupitia matayarisho ya mpango wa menejimenti ya Mazingira kwa maeneo yaliyo chini (na maeneo mengine muhimu kwa baioanuwai) ya wilaya ya Rufiji – kwa kutilia mkazo misitu na sehemu zake zenye miti na chepechepe pamoja na kuwashirikisha washikadau WOTE katika utaratibu wa mipango.

2. Pima na halafu tekeleza Mpango wa Menejimenti ya Mazingira kwa wilaya ya Rufiji pamoja na kuwashirikisha mamlaka na jamii za Wilaya na wakati huohuo kuvisaidia vijiji vya mfano kuendeleza na kutekeleza mipango ya menejimenti ya mazingira ya jamii kwa maliasili za maeneohusika.

Mpaka sasa mradi umefanya kazi kwa karibu miaka miwili. Katika kipindi hiki, mkazo umekuwa katika kufanya tathmini mbalimbali za kiikolojia na uchumi wa kijamii ili kuboresha welewa wa hali zao. Kama sehemu za tathmini za maliasili utafiti mbalimbali umefanywa kuanzia uchunguzi toka angani na kazi za GIS, orodha ya baioanuwai, tathmini ya hadhi ya sasa ya maliasili za mbao katika maeneo ya miti, na mabadiliko ya chepechepe.

Kwa tathmini za hali ya uchumi wa kijamii, mradi umeshafanya utafiti wa vijiji vinne vya mfano, na kwa sasa tuko katika utaratibu wa kutathmini vijiji kumi zaidi.

Kuna miradi mingine wilayani Rufiji ambayo tunashirikiana nayo na ambayo inachangia kwenye menejimenti ya maliasili wilayani. Kwa hiyo kwa sasa kuna taarifa za kutosha kuwezesha uundaji wa rasimu ya Mpango wa Menejimenti ya Mazingira.

Jambo muhimu kwa mradi ni utaratibu wa maendeleo ya Mpango wa Menejimenti ya Mazingira, ambao ni lazima uendeshwe katika njia ya ushirikishaji, ili kuhakikisha kuwa endelevu . Hii itahitajika kufanya kazi kwa karibu na washikadau wote katika ngazi ya Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa.

Hatimaye, makundi ya washikadau yafuatayo yalialikwa katika warsha hii ya mpango wa menejimenti wa mazingira wa kwanza kujadili juu ya masuala ambayo yanahitaji kufikiriwa wakati wa uelezaji wa Mpango wa Menejimenti ya Mazingira wa Wilayani ya Rufiji (), wafanyakazi wa Wilaya ya Rufiji, madiwani wa Wilaya ya Rufiji, wafanyakazi wa tarafa, wafanyakazi wa kata, wawakilishi wa jamii wilayani, miradi mingine/ taasisi katika wilaya ya Rufiji, makundi yanayotumia maliasili mbalimbali, na vyama visivyo vya kiserikali(NGOs).

Katika kipindi cha kuingilia kati Mpango wa Menejimenti ya Mazingira wa Wilaya (EMP), umekuwa ukiunganisha taarifa zilizopatikana toka kwenye utafiti wao wenyewe na ule wa utafiti uliotangulia na kuzichambua taarifa hizo ili kuziingiza katika utaratibu wa Mpango wa Menejimenti ya Mazingira. Inafikiriwa kuwa warsha ya pili ya washikadau ambayo itashirikisha makundi ya washikadau kama ilivyobainishwa katika warsha hii, itapangwa hivi karibuni.

Ripoti ya Warsha ya Mpango wa Menejimenti ya Mazingira wa Wilaya ya Rufiji – Juni 29-3-, 2000.
Warsha hii imefanikiwa katika malengo mawili.

1. Kwanza kuwatambua washikadau wanaofaa katika ngazi ya eneo husika, wilaya, mkoa na taifa, aidha, kupanga utaratibu wa mpango unaoweza kubadilika kulingana na hali halisi ambao ndio utakaofuatwa.

2. Pili imezaa masuala muhimu ya menejimenti na maliasili ambayo yanahitaji kufikiriwa katika kubuni mpango wa menejimenti wa mazingira kwa Wilaya ya Rufiji. Kwa hiyo uendeshaji huu wa warsha utaunda msingi muhimu katika utaratibu wa EMP.

Inategemewa kuwa warsha itakayofuata itaweza kubainisha masuala zaidi yatakayoshughulikiwa katika utaratibu wa EMP, na kutoa mwanga wa manufaa kwa mengine ambayo yanaweza kuwa yamesahauliwa wakati wa warsha ya kwanza. Ni dhahiri kuwa mfumo wa menejimenti kwa maliasili katika Wilaya ya Rufiji ni wamuhimu, na moja ya malengo ya warsha inayokuja haina budi kuyajadili malengo ya utaratibu wa menejimenti, yale ya muda mrefu na ya kiutendaji.

# 2 Ufunguzi

**Bw. Isa Lembuya (Mkuu wa Wilaya ya Rufiji)** iliyosomwa kwa niaba yake na Katibu Tawala wa Wilaya.

Warsha ilifunguliwa na MKUU wa wilaya, ambaye aliwakumbusha washiriki wa warsha kuwa Mradi wa Menejimenti ya Mazingira wa Rufiji ilikuwa ni shughuli ya pamoja kati ya washikadau mbalimbali pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kama wakala mkuu wa utekelezaji ikishirikiana na vyama

vingine katika ngazi ya mkoa na taifa, na kupata msaada wa kiufundi toka UHD - Umoja wa Hifadhi Duniani. Alisisitiza tena na tena kuwa mradi uko katika awamu yake ya kwanza, na awamu nyingine kadhaa zinatarajiwa, hiyo itaimarisha shughuli ambazo zimeanzishwa hivi sasa. Cha muhimu sana kwa wakazi wa wilaya ya Rufiji, ni mwenendo wa kujishughulisha. Katika kuweka uwiano kati ya hifadhi na mahitaji ya maendeleo, pamoja na shabaha ya msingi ya kuboresha viwango vya maisha yao.

Ingawa wilaya hii imejaliwa kwa kuwa na utajiri wa kuanzia misitu kama milima ya Kichi, Namakutwa-Nyamuete, Mchungu, rasilimali za sehemu chepechepe katika tambarare za mafuriko na delta zenye rasilimali anuai za uvuvi na mikoko, shinikizo toka ukuaji wa idadi ya watu, ukataji magogo, kilimo, shughuli za uvuvi usio endelevu, uharibifu wa maji, na uharibifu wa maji, na uharibifu wa mikoko vinaongezeka, na kulazimisha uundaji wa Mpango wa Menejimenti ya Mazingira. Mkuu wa Wilaya (MW) alikazia kuwa kuendeleza mikakati ya kimatendo kuwa matumizi na hifadhi ya mali asili ni njia mojawapo ya kusonga mbele. Alizisifu shughuli za Mradi wa Menejimenti ya Mazingira wa Rufiji katika vijiji vinne vya mfano vya Jaja, Mbunju Mvuleni, Mtanza Msona na Twasalie, na akapendekeza kuwa hapo baadaye njia za kushirikisha menejimenti ya maliasili itumike pia kwa eneo lote la mradi lililobaki.

Ushirikishaji wa wwashikadau wote wanaofaa, kwa kuzingatia uchaguzi na maendeleo ya mikakati ya hifadhi ya baioanuai juu ya taarifa bora ya kitaalam inayokusanywa kutokana na utafiti unaoendelea katika maliasili na vipimo vya uchumi wa kijamii, na ushirikiano wa karibu na miradi na taasisi nyingine vyote ni vitu muhimu kwa ufafanuzi wa Mpango wa Menejimenti wa Mazingira. MW aliwatakia washiriki wa warsha mkutano wenye mafanikio, akiwashauri kuwa ikiwa mpango unaofikiriwa utaendeshwa vizuri hautakuwa umehakikisha kuendelea kufaidika kutokana na huduma na mazao toka kwenye maliasili zao kwa vizazi vya sasa tu, bali hata kwa vizazi vijavyo.

**Makaribisho toka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji**
**Bw.Chande-Afisa Ardhi, Mali Asili na Mazingira wa Wilaya.**

Bw. Chande aliwakaribisha washiriki wa warsha kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji. Bw. Chande aliwakumbusha washiriki wa warsha kuhusu matunda yanayotegemewa ya mradi, kuu kati ya hayo ikiwa ni Mpango wa Menejimenti ya Mazingira wa Wilaya na mengine yakiwa ni Mpango wa Menejimenti ya Mazingira wa Kijiji, udumishaji wa misitu muhimu, na uwezo ulioboreshwa katika wilaya ya Rufiji wa kupanga kuhusu matumizi ya maliasili kwa msingi wa mfumo wa ikolojia.

**Utaratibu wa Mpango wa Menejimenti ya Mazingira Uliopendekezwa**

Alieleza zaidi utaratibu wa mpango wa mazingira uliofikiriwa na wilaya inabidi uwe wa kushirikisha kadri iwezekanavyo ili kuhakikisha kuwa washikadau wote wanaelewa na kuchangia muundo, utekelezaji na urekebishaji wa mara kwa mara kulingana na hali au wakati.

**Hali ya sasa**

Katika miaka miwili iliyopita mradi umekuwa ulijishughulisha zaidi na kukusanya na kuimarisha taarifa kuhusu mambo mbalimbali kama vile ya kiikolojia, kijamii, na uchumi katika kulingana na sheria zilizopo.

Katika miezi ijayo taarifa hii itapitiwa na kuchambuliwa ili kusisitiza mambo mazuri na mabaya ya matumizi ya maliasili na athari zake. Nyingi ya taarifa za kiufundi zilizokusanywa miaka miwili iliyopita zimetoka kwa washauri waliotumwa na mradi. Tafadhali rejea karatasi iliyoambatanishwa kuhusu washauri mbalimbali waliohusika mpaka sasa na waliobaki. Pamoja na washauri, mradi pia umekusanya taarifa za msingi toka kwa wafanyakazi wa wilaya. Taarifa hizi ni kutokea utafiti wa uvuvi unaoendelea, utafiti wa muundo wa ukataji magogo, takwimu za mifugo, utaratibu wa mpango wa menejimenti ya mazingira wa kijiji ambao umeupatia mradi taarifa muhimu sana katika hadhi ya maliasili vigezo vya uchumi wa kijamii katika vijiji vya majaribio vinavyohusika. Mwisho, miradi mingine ndani na nje ya eneo la mradi imechangia taarifa zao na mradi wa menejimeti ya mazingira wa Rufiji, ambapo nyingine kati ya hzo zitafaa kwa muundo wa EMP. Kwa sasa, mradi wa menejimenti

ya mazingira unatayarisha ambatanisho la bibliografia ya utafiti wote uliotangulia (ikolojia, haidrolojia, uchumi wa kijamii) yakiwemo na maendeleo ya juu auya chini.

Menejimenti imeanzisha utaratibu wa kubuni Mradi wa Menejimenti ya Mazingira kwa ukanda wa Mafuriko wa Rufiji na Delta. Muhimu kwa utaratibu mzima ni kuhakikisha ushiriki wa shikadau wote katika ngazi zote (Kijiji, Kata, Tarafa ,Wilaya, Mkoa na Taifa), tunafikiri kuwa utaratibu huu ungemalizika mnamo miezi sita ijayo.

Vipengele vya hapo chini vinaelezea kwa mapana utaratibu wa uundaji wa mpango wa menejimenti ya mazingira uliofikiriwa.

1. **Upitiaji na uchambuzi wa taarifa iliyopatikana:** Mkazo utakuwa kuchambua taarifa yote iliyopatikana, kutambua shughuli zinazoendelea kufanywa na washikadau mbalimbali, na kufanya upitiaji wa utaratibu uliopo na unaoendelea katika eneo la mradi, Wilaya ya Rufiji na eneo la Bonde la Mto Rufiji.

2. **Ushirikishaji washikadau** (wa ndani) Wilayani Rufiji katika utaratibu wa Mpango wa Menejimenti. Washikadau kwa kiasi kikubwa watachukuliwa toka vijijini, kata, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, vikundi mbalimbali vinavyotumia maliasili (kuanzia wavuvi, wakataji magogo, wapasua mbao, kampuni za wavumbuzi wa mafuta, n.k.), wafanyakazi wa Wilaya ya Rufiji, Vyama Visivyo vya Kiserikali, miradi ya hifadhi na maendeleo kwa kutaja vichache. Ushauri katika hatua hii utahusisha warsha ya kushauriana kujadili maswala mengi ya menejimenti ya maliasili na chaguo za menejimenti. Baada ya warsha kutakuwa na juhudi zitakazoelekezwa kwenye ufuatiliaji wa maswala ya menejimenti yaliyoibuka ama katika ngazi za kijiji, kata ya sehemu yoyote inayostahili na watumiaji wa maliasili maalum, miradi mingine, Halmashauri ya Wilaya, n.k. Ushirikishaji wa jamii za ndani katika ngazi za chini (vijiji, na kata) umekuwa ukiendelea katika vijiji vingi vya maeneo ya mradi, lakini msisitizo ukiwa zaidi katika vile vijiji vinne vya mfano.

3. **Ushirikishaji wa Serikali za Wilaya, Mkoa na Serikali Kuu**. Mradi umekuwa ukishirikiana na taasisi na idara kadhaa katika ngazi za Taifa na Mkoa. Hizi ni kuanzia misitu na kitengo cha ufugaji, nyuki, NEMC, Tume ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Taifa, Taasisi ya Tathmini ya Rasilimali, Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Vyama Visivyo vya Kiserikali vya Taifa, kama Chama cha Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania(CUWT), WWF na miradi mingine katika Bonde la Mto Rufiji. Warsha ya pili ya kushauriana itapangwa kwa majaribio Novemba 2000. Madhumuni ya warsha maalumu itakuwa ni kujadili na kuboresha maswala ya Menejimenti na chaguo za menejimenti ambazo zitaibuka wakati wa warsha ya kwanza ya washikadau wa Wilaya. Inafikiriwa kuwa warsha pia itabainisha mikakati mipana ambayo itatumika kukuza menejimenti za rasilimali zilizounganishwa na kupunguza uwezekano wa mgogoro wa matumizi ya ardhi.

4. **Warsha za kiufundi**: kujaza mapengo yaliyobainishwa. Ni dhahiri kuwa vipengele 1,2,3 vitabainisha mapengo yanayohusiana na vipengele mbalimbali vya mradi. Kwa kuzingatia msingi huu warsha2 za kiufundi zitaandaliwa. Kwa mfano uanzishaji wa utaratibu wa tathmini ya athari ya mazingira ambao ungeweza kuongozwa na NEMC, kubuni matumizi ya ardhi na mpango wa maendeleo kikanda ambao ungeweza kuongozwa na Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Uunganishaji wa kufuata mkondo na kupingana na mkondo wa mto kwa lengo la kubainisha chaguo za menejimenti pana ya chanzo cha mto, n.k.

5. **Mwendelezo wa rasimu ya Mpango wa Menejimenti ya Mazingira**: Hatua 1 mpaka ya 4 zitakusanya taarifa ya kutosha kuiwezesha timu ya menejimenti ya mazingira ya Wilaya (TMM) kuendeleza rasimu ya mpango wa menejimenti ya mazingira kwa uwanda wa mafuriko na delta ya Mto Rufiji. Taarifa yoyote mpya itakayopokewa kati ya sasa na baadaye itaingizwa katika mpango. Mpango baadaye utasambazwa kwa washikadau waliotambulika kwa hoja zao na ushauri wa kwa uboreshaji. TMW inapanga kuwa na rasimu ya EMP tayari ifikapo Desemba.

6. **Mikutano ya kushauriana kuhusu kujadili EMP**: Hoja zilizopokewa toka kwa washikadau zitakusanywa, kuchambuliwa na kujadiliwa katika warsha hii. Kwa kuzingatia hoja hizi rasimu ya EMP zitapitiwa tena ipasavyo na kusambazwa kwa washikadau wanaohusika ifikapo Desemba 2000.

7. **Majaribio ya Mpango wa Menejimenti ya Mazingira** katika awamu ifuatayo (miaka 3).

8. **Kurekebisha** EMP kulingana na mafunzo yaliyopatikana.

Washiriki wa warsha walivichukua vipengele vya juu kama utaratibu wa kimantiki kwa maendeleo ya Mpango wa Menejimenti ya Mazingira ya Wilaya.

# 3 Utaratibu Mwingine wa Maendeleo ya Mipango ya Menejimenti ya Maliasili

Timu ya mipango ya mazingira wilayani Rufiji (EMT) ilialika miradi mingine kadhaa toka ndani na nje ya Wilaya ya Rufiji kubadilishana uzoefu wao jinsi walivyoendeleza na kutelekeza Mipango wa Menejimenti ya Maliasili. Ilionekana kuwa muhimu kwa washiriki wa warsha kuelewa maana na matokeo ya kuwa na Mpango wa Menejimenti ya Mazingira.

Mwishoni EMT ilimwalika Afisa wa Maliasili wa Wilaya ya Kilosa toka Wilaya ya Kilosa ambaye hapo nyuma aliongoza utaratibu wa mpango ambao unatekelezwa katika Wilaya ya Rufiji. Taarifa kutoka katika miradi mitatu ya wilaya ya Rufiji na mmoja kutoka wilaya ya Kilosa ilitoa mwanga kwa washiriki wa warsha kuhusu jinsi mpango huu ulivyoendeshwa katika maeneo tofauti na kwa maliasili mbalimbali. Hii ni muhimu sana kwa miradi yenye mipango ya menejimenti iliyomo wilayani Rufiji, kwa kuwa mipango yote hii ya menejimenti inabidi iunganishwe kuwa mpango mmoja wa jumla wa menejimenti ya Mazingira kwa ajili ya wilaya.

**PROGRAMU YA MAENDELELO YA WILAYA YA KILOSA MPANGO WA WILAYA WA MIAKA MITATU (1998-2000)**

**Bw. Musa Zungiza (Afisa wa Maliasili wa Wilaya-Wilaya ya Kilosa)**

Bw.Zungiza alieleza kuwa utaratibu huu uliotumika au kuchaguliwa kuendeleza mpango wa miaka mitatu wa wilaya ulikuwa njia ya mpango wa umoja wa Ulaya wa ushirikishwaji wa menejimenti ya mlolongo wa miradi ya umoja wa wilaya ikiwemo Mbinu ya Uchambuzi wa Msingi wa Kimantiki. Kwa jumla matatizo 257 yalibainishwa na kupangwa. Hizi zilizingatia uzoefu wa wakazi wenyeji (wanakijiji), uzoefu wa wafanyakazi wa Halmashauri ya Kilosa, washauri wa programu, matokeo ya washauri na mazoezi ya PRA. Baadaye matatizo yalipangwa katika sekta zinazohusika na kuundwa tena katika malengo. Upangaji malengo katika maeneo husika yanayoungana yalifanyika. Hizi baadaye zilipewa kipaumbele katika upangaji kulingana na umuhimu wao unaojitokeza kupitia zoezi la kimadaraka. Zaidi ya watu 60 kutokea wataalam, washauri, wawakilishi wa jumuia za ndani, wafugaji, wabunge, madiwani, Vyama Visivyo vya Kiserikali na viongozi wa dini walioshiriki katika ubainishaji na utambuzi wa matatizo. Pia mpango huu utashirikisha matokeo, shughuli, dhana na masharti ya awali ya nyongeza.

Jinsi muda ulivyokuwa unakwenda udhaifu ufuatao wa mpango umetambulika: matokeo yenye matarajio; malengo ambayo hayawezi kupatikana mf. Upunguzaji wa moto kwa 60% katika miaka; Upunguzaji ukataji miti haramu kwa asilimia fulani wakati hakuna data wala takwimu zilizofanywa (taarifa ya kimsingi inakosekana); uratibu wa kikamilifu kati ya sekta mbalimbali haupo. Ingawa wafanyakazi kutoka idara moja wanafanya kazi na wa idara nyingine wakati wa utekelezaji wa shughuli; na mwishowe utaratibu kati ya mawakala kwa matumizi bora ya rasilimali haukufafanuliwa vizuri.

Kwa kuhitimisha Bw. Zungiza alieleza zaidi haja ya kushirikisha washikadau wahusika hasa wanajamii ambao kwa kawaida wana mchango mkubwa katika maliasili na wataathirika zaidi (vibaya) na kazi za maendeleo za kiwango kikubwa. Ukosefu wa taarifa sahihi kuhusu hadhi ya maliasili pia unaweza ukazuia utaratibu wa mpango.

**MPANGO WA MENEJIMENTI WA MIKOKO WA TAIFA**

**Bw. Gasper Levira**

Bw. Levira aliwataarifu washiriki wa warsha kuhusu mpango wa Menejimenti ya Mikoko wa Taifa, na kuhusu mradi unavyotekeleza mpango ambao uko katika awamu yake ya pili na ambao utamalizika mwaka 2004. Mpango wa Menejimenti ya Mikoko wa Taifa ulianzishwa baada ya upigaji picha toka hewani na zoezi kamili la utafiti ardhni lilisababisha uainishaji wa kanda nne za menejimenti. Kanda hizi za menejimenti ni misitu inayopata hifadhi kamili, misitu itakayowekwa chini ya uzalishaji, maeneo yasiyofaa ambayo hayatatumika kuruhusu urejeshi na utumiaji upya na maeneo ambayo yatatengwa kwa maendeleo ya aina mbalimbali.

Alieleza kwamba utaratibu wa mpango wa menejimenti ya mikoko ni mfano wa hali ya juu ambapo taarifa ya kiufundi haishikamanishwi na matarajio ya kiuchumi wa jamii wa wanajamii wa kawaida kitu ambacho ndicho kilichokuwa udhaifu wa mpango. Alitoa mfano wa delta ambayo ni pana sana na utawala wa mradi hauna vifaa vya kufanyia doria ya mara kwa mara. Kama wanajumuia wa kawaida na washikadau wengine wangeshirikishwa toka mwanzo mradi ungekuwa na mafanikio bora ya kuonyesha katika miaka 4-5 ambayo umekuwa ukifanya kazi . Kwa kutambua mapungufu haya, mradi wa Menejimenti ya Mikoko umetambua haja ya kuwashirikisha wanajamii wa kawaida na inafanyia majaribio njia mbalimbali shirikivu za umenejimenti ambazo zimekwisha anzishwa katika eneo la Tanga. Katika Delta ya Rufiji, EMP unafanya kazi kwa karibu na EMP katika vijiji vya majaribio vilivyounganishwa vya

Jaja na Twasalie na vijiji vinane vingine. Kwa kuhitimisha Ndugu Levira alisema kwamba utiliaji mkazo wa kupita kiasi wa jambo moja au zaidi ungeharibu mingine, na kuwa uwiano wa kufaa wa taarifa ya kiufundi na ile ya uchumi wa kijamii ni muhimu.

**USHIRIKISHAJI WA WWF KWENYE UHIFADHI WA BAIOANUWAI NCHINI TANZANIA**
**Bw. Cyprian Malima**

Bw. Malima aliwataarifu washiriki wa warsha kuwa kazi ya WWF inaendeshwa na shauku ya kuwa na dunia asilia iliyoegemezwa kwenye Sayansi na kupewa sura kwa kuelewa kuwa kushughulikia mahitaji ya binadamu ni jambo muhimu sana kwa mafanikio ya uhifadhi wa muda mrefu. Ili kukabiliana na changamoto hii, WWF inatumia njia ambazo zinatofautiana kama vile mahitaji ya changamoto inavyotaka kuanzia kwenye kubuni na kuimarisha Mbuga na sehemu zilizohifadhiwa hadi kwenye kuingiza uhifadhi kwenye utaratibu wa maendeleo ya uchumi wa ndani, toka kwenye kulinda viumbe vilivyo hatarini hadi kwenye kuhamasisha sera za kimazingira za dunia.

Toka ofisi ya WWF ilipofunguliwa, programu imeongezeka toka miradi mitano hadi miradi 15 inayofanya kazi. Alielezea zaidi kuwa misitu ya uwanda wa chini wa pwani kama ile inayopatikana katika Wilaya ya Rufiji inatunza mkusanyiko wa wanyama na mimea (‘fiona’ na ‘flora’) wa kipekee na tofauti katika mazingira, vitu vinavyotoa mazao mbalimbali ya misitu kwa ajili ya wanajamii wa kawaida. Misitu ya Pwani imo kwenye tishio tokana na shughuli za binadamu kama vile kilimo cha kuhamahama, ukusanyaji mbao za kuni, ukataji miti, utengenezaji mkaa, uvunaji wa mbao, mioto ya vichaka, na uchimbaji madini. WWF imekuwa ikipigania upatikanaji wa uhifadhi na maendeleo ya wanajamii wa kawaida kupitia kwenye matumizi ya kudumu ya vifaa vya majini. Shughuli zinalenga katika kufanya kazi na wanajamii wa Mafia ili kuboresha matendo ya maendeleo na viungo vya utoaji maamuzi, kuimarisha ushiriki wa wanajamii wa Mafia, kuimarisha miundombinu na wafanyakazi, na kutoa msingi wa menejimenti wa kila siku kwa ajili ya Mbuga.

Kwa kushiriki ana na GTZ/SCP, vijiji viwili(Ngarambe wa Tapika) vya wilaya ya Rufiji vimeingizwa katika Mpango wa Uhifadhi wa Wanyamapori wa Selous wa menejimenti na Uhifadhi wa WWF. Vijiji hivi kupitia kwenye kamati yao ya maliasili iliyochaguliwa na maskauti wa Wanyamapori wa Kijiji walioteuliwa sasa wanamiliki maliasili zinazojitokeza katika eneo lao la kisheria. Maskauti wa wanyamapori wa kijiji huendesha doria na kukagua uwindaji wa nyama za pori katika maeneo husika ya menejimenti ya wanyamapori. Mapato yanayopatikana tokana na matumizi ya wanyama pori yanatumika kukidhi baadhi ya miradi ya maendeleo ya kijiji kama vile ukarabati wa nyumba ya Mwalimu Mkuu na madarasa ya shule ya msingi n.k Kutokana na uzoefu wa WWF katika uhifadhi wa viumbe anuai, Bw. Malima alipendekeza kuwa hatua za upangaji za uhifadhi wa mazingira lazima zijumuishe ushirikishwaji wa washikadau wote na maendeleo ya wanajamii wa kawaida.

**HATUA ZA MPANGO WA MENEJIMENTI YA HIFADHI YA WANYAMAPORI YA SELOUS NA MAFUNZO YALIYOPATIKANA TOKANA NA UHUSISHAJI WA VIJIJI VYA MAJARIBIO.**
**Bw. Rudolf Hahn.**

Bw. Hahn alieleza kuwa hatua za maendeleo ya mfumo wa Menejimenti ya Hifadhi ya Wanyama pori ya Selous ina umri wa miaka 10. Msingi wa Hifadhi kutegemea Jamii (HKJ) / Mradi wa Hifadhi wa Selou (MHS) unachukua hatua kadhaa na ni wa hatua ndefu. Uzoefu wa kimatendo unaonyesha kuwa ni ndoto kuchukua kijiji kimoja pekee toka kwenye mfumo wa ikolojia na kujaribu kutekeleza kwa kutumia kijiji hiki menejimenti ya maliasili ya kudumu. Kwa ukweli wanajamii au makundi ya watumiaji wa maliasili hutumia maliasili hizo toka kwenye mfumo mmoja wa ikolojia. Alitoa mfano wa majangili wa nyama ambao hawafanyi ujangili katika maeneo ya vijiji vyao wenyewe bali watafanya ujangili popote wanyamapori wanapopatikana kwa urahisi. Kwa hiyo kama kijiji kimoja pekee kitaanzisha Eneo la Menejimenti ya Wanyamapori (EMW ), kitapata matatizo ya kudumu na majangili toka vijiji jirani. Pia kiuchumi ni vigumu kushughulikia kijiji kimoja cha mfumo mmoja wa ikolojia. Tayari inaanza na upimaji wa mpaka wa kijiji-vijiji vyote vya jirani itabidi visaini mkataba wa maelewano kuhusiana na mipaka ya kijiji kimoja maalum. Ikiendelea na matumizi, kwa mfano EMW ya kijiji kimoja inaweza kuwa ndogo sana kiasi cha kutoweza kuwa kizuizi cha kufaa kwa uwindaji au hakina uwezo wa kupata maji (ambapo ina maana wanyama hukaa kwa msimu tu katika eneo hilo). Ili kupata faida ya juu zaidi toka kwenye eneo hili menejimenti unganifu pamoja na vijiji kadhaa itakuwa ni ya muhimu. Na itabidi uthibitishwe kuwa uhifadhi ni wa faida zaidi kuliko matumizi mengine ya ardhi.

Maelezo haya kwa hakika yanahusu menejimenti ya wanyamapori na hayakuwekwa wazi zaidi. Kuhusu Misitu au Uvuvi itakuwa ni jambo tofauti tena. Baada ya kugawa eneo lako lote la mradi, ambalo ni la aina mbalimbali katika mifumo ya ikolojia yenye kufanana kuhusu umuhimu na matumizi, utagundua kuwa vijiji vinavyoshirikiana mpaka na Hifadhi ya Wanyama pori ya Selous vina umuhimu wa juu wa aina moja na pia matatizo. Alishauri kutoa maombi kwa vijiji vyote hivi kuwa na uwezekano wa kuanzisha EMW ili kuhifadhi maliasili. Kwenye delta, kama haijafanyika bado inabidi ujaribu kuanzisha takriban eneo moja mahsusi linaloundwa kikamilifu pale ambapo utalii wa kiikolojia unaweza kugharimia gharama za ulinzi na manufaa kwa wananchi wa kawaida.

**HATUA ZA MPANGO WA MENEJIMENTI YA MAZINGIRA WA KIJIJI WA EMPK (Mpango wa Menejimenti wa Mazingira wa Kijiji)**
**Bi Pili Mwambeso**

Bi Mwambeso alidokeza hatua zilizotumika katika uteuzi wa vijiji 4 vya majaribio vya Jaja, Twasalie, MbunjuMvuleni na MtanzaMsona, na maendeleo ambayo vijiji hivi vimefanya katika kueleza mipango ya menejimenti ya mazingira ya kijiji husika.

Alitoa taarifa kuwa hatua ya I (kuanzisha taarifa ya msingi) ilihusu kujifunza juu ya VEMP toka kwenye vijiji juu ya jinsi wanavyotumia ardhi, maliasili na kuendesha mafunzo ya uchumi wa kijamii ili kupata taarifa juu ya baadhi ya familia, maliasili ambazo wanazimiliki, matumizi ya maliasili katika maeneo husika, mipaka ya vijiji husika, shughuli muhimu za kiuchumi na idadi ya watu wanaoweza kufanya kazi. Hatua ya II ilihusu utambuzi wa matatizo na uchaguzi wa timu ya menejimenti ya mazingira kuongoza hatua za upangaji. Hatua III iliangalia juu ya malengo ya maendeleo kwa ajili ya Mpango wa Menejimenti ya Mazingira wa Kijiji (EMPK) kwa kukabiliana na matatizo yaliyotambuliwa, na kwa hatua ya IV ni kutambua mikakati mbalimbali ya kutumia. Timu ya mipango ya baadaye iliendeleza EMPK, ambayo inabidi ithibitishwe katika ngazi ya Kijiji, Kata na Wilaya. Hatua ya mwisho ni utekelezaji na uboreshaji wa EMPK.

# 4 Uchambuzi wa Washikadau

**Iliwezeshwa na Msimamizi wa Warsha mwenye mamlaka.**

Kutokana na taarifa ya utaratibu wa mpango wa menejimenti wa maliasili moja ya maswala muhimu ambalo limejitokeza sana lilikuwa washikadau – kutambulika kwao na ushirikishwaji wa mpango wowote wa menejimenti ikiwa ni kwa mfumo wa ikolojia, eneo maalum, na ikiwa kwa vyama vya kiserikali au visivyo vya kiserikali. Vikundi vya washikadau vinaweza kujumuisha jamii husika inayotumia – jamii za pembeni za msitu, jamii za wenyeji zilizo na shauku zisizo wazi. Menejimenti ya rasilimali- kwa kutegemea kazi fulani za maliasili, kwa mfano, ugavi wa maji, jamii za mbali zinazotumia maliasili, kwa mfano watalii ambao mara kwa mara hutembelea Rufiji, mawakala wa serikali (ya mtaa, kuu, mashirika ya umma, taasisi za taifa zilizopewa mamlaka na menejimenti ya maliasili nchini), na vyama vya mazingira na Uhifadhi, vya ndani, taifa, mkoa na kitaifa.

Makundi ya washikadau wafuatao yalitambuliwa ndani ya mamlaka na kupendekezwa kuhusishwa katika maendeleo ya mpango wa menejimenti ya mazingira kwa ajili ya Wilaya ya Rufiji.

## 4.1 Vikundi vitumiavyo Maliasili vya ndani

| Kundi litumialo maliasili | Aina ya maliasili | Mahali |
|---|---|---|
| Jamii ya wavuvi | Samaki –wa magamba na wa mapezi, viboko, kamba, n.k. | Bahari, mito, vidimbwi, maziwa. |
| Wachuuzi wa ukindu | Majani ya Ukindu | Hasa katika delta. |
| Wawindaji (chama cha uwindaji) | Wanyama wa porini, Ndege | Delta, Uwanda wa mafuriko, Nyanda za juu. |
| Wavunaji mbao/<br>Wakataji magogo | Miti, boriti | Delta, Uwanda wa Mafuriko, misitu ya Nyanda za juu kama milima ya kichi, Ngulakula, n.k |
| Wavunaji/Wakataji mikoko | Boriti za mikoko | Delta. |
| Mafundi seremala | Mbao | Katikati ya miji |
| Mashirika ya uchimbaji madini | Mafuta na Gesi | Delta, na Nyanda za juu katika Kisangire, Kisiwa cha Songo Songo. |
| Wachuuzi/Wanunuzi wa kamba | Kamba | Delta. |
| Waendeshaji utalii | Utalii-wanyama pori | Kambi/Nyumba za kulala wageni katika Hifadhi ya wanyama ya Selous |
| Warinaji asali | Miti ya kutengenezea mizinga | Delta, Uwanda wa mafuriko, Nyanda za juu. |
| Watengenezaji/Wachuuzi wa mkaa | Miti- kutengeneza mkaa | Kuenea katika wilaya nzima. |
| Wafanyakazi wa machimboni | Mawe, Mchanga, | Mto Rufiji, Nyanda za juu. |
| Wakulima na wafugaji ng'ombe | Ardhi, misitu, maji, nyasi kavu | Delta, Uwanda wa mafuriko, Nyanda za juu. |
| Waganga wa kienyeji | Miti, nyasi, maji, asali, wanyama wa porini, ndege | Delta, uwanda wa mafuriko, Nyanda za juu. |
| Wajenzi | Udongo wa ardhi, miti, maji, mawe | Delta, uwanda wa mafuriko, Nyanda za juu. |

**Idara za serikali na taasisi zilizopewa madaraka na mamlaka ya menejimenti ya maliasili na katika ngazi za Wilaya, Mkoa na Taifa**

- Idara za menejimenti maliasili: kilimo na mifugo, Ardhi, Maji, Uvuvi, Misitu, Hifadhi katika ngazi za Wilaya na Mkoa.
- Kamati ya mazingira na Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji (ikiundwa na madiwani wa kuchaguliwa)
- Wizara ya maliasili na Utalii katika ngazi ya Taifa

- Wizara ya Kilimo
- Wizara ya Nishati (Kitengo cha madini)
- Baraza la Menejimenti ya Mazingira ya Taifa (BMKT)
- Tume ya mpango wa Matumizi ya Ardhi (TMMA)
- Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Mto Rufiji (RUBADA)
- Ofisi ya Maji ya Bonde la Mto Rufiji (OMMR)
- Mradi wa Menejimenti ya Bonde la Rufiji na Uboreshaji Umwagiliaji wa Vishamba Nidogovidogo (MMBRUUV)
- Wizara ya Fedha – Tume ya Mipango
- Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania
- Idara ya Uhandisi Ujenzi ya Wilaya (Ujenzi wa barabara na madaraja) na miradi ya uboreshaji barabara na madaraja na miradi ya uboreshaji barabara katika ngazi za kijiji na wilaya.
- Wizara ya Serikali ya Mitaa na Tawala za Mikoa

**Vyama Visivyo vya Kiserikali**

- Rufidelta
- Wakala wa Maendeleo ya Mloka Mkongo
- Chama cha Hifadhi ya Wanyama Pori Tanzania(CHWT)

**Miradi mingine ya Menejimenti ya Maliasili Wilayani Rufiji na maeneo yanayozunguka**

- Mradi wa Ufugaji nyuki Rufiji (MUNR)
- Mradi wa menejimenti ya Mikoko (EMPK)
- Miradi ya Hifadhi ya misitu ya Pwani ya WWF na Menejimenti ya Wanyamapori
- Programu ya Hifadhi ya Selous GTZ- mradi wa Hifadhi inayotegemea jamii katika Tapika na Ngarambe
- Mbuga ya Taifa ya Mafia Island Marine
- Mradi wa Menejimenti ya Pwani Tanzania (MMPT)

**Kampuni zenye mwelekeo wa kibiashara (toka nje ya Wilaya ya Rufiji)**

- Kampuni ya Uvuvi ya Kiafrika (KUA) –Uvuaji kamba katika Delta
- SONGAS (Uchimbaji gesi katika kiwanda cha Songosongo
- Waendeshaji Hoteli na Utalii
- Chama cha Uwindaji
- Waendeshaji Kikokoozi na Wachuuzi wa Rasilimali za Uvuvi.

Ilipendekezwa kuwa inabidi makundi ya washikadau hapo juu yashirikishwe katika utaratibu wa mpango wa menejimenti, ushirikishwaji wa makundi hayo uonekane kama manufaa ya ziada kwani wataweza kutoa utaalamu wao kama vile kuhusu sheria na maswala ya sera ambayo yanaweza kuwa yanakosekana katika wilaya.

# 5 Majadiliano ya Vikundi

Washiriki waligawanywa katika vikundi vinne kujadili masuala mbalimbali yanayoathiri menejimenti ya kudumu ya maliasili maalum. Vikundi vilizingatia maliasili kuu/matumizi makuu ya ardhi kwa wilaya ya Rufiji. Hizi ni misitu, uvuvi, kilimo, na wanyamapori (wakiwemo wa uwindaji na utalii). Washiriki walitakiwa kujiunga na vikundi ambavyo walijisikia wangeweza kuchangia zaidi kwa kuzingatia utaalam/ utumiaji wao. Kila kikundi kilitakiwa kuorodhesha shughuli katika sekta husika ya maliasili, na kutaja bayana ilitokea wapi, na kujadili na kuorodhesha masuala ya menejimenti yanayohitaji kushughulikiwa katika menejimenti ya mazingira ili yaendelezwe hapo baadaye. Haya ni baadhi ya masuala ya menejimenti ambayo utaratibu wa maendeleo ya mpango wa menejimenti utajaribu kuyashughulikia. Matokeo ya shughuli za vikundi hivyo yanaonyeshwa hapo chini.

Kila kikundi kilipewa fomu zinazoonyesha matumizi/ eneo analomiliki ili wilaya iweze kuonyesha kwa kutumia maeneo yaliyoathiriwa na shughuli/ uingiliwaji wao kisha kila kikundi kilitakiwa kuorodhesha masuala yote ya menejimenti yanayotumika kama vile haki, leseni, upatikanaji, upungufu, ushuru, uharibifu n.k. Vikundi viliwakilisha majadiliano yao kwenye mamlaka kwa njia ya ramani na orodha ya masuala.

## 5.1 Kikundi cha Kilimo

| SHUGHULI | ENEO | MASUALA YA MENEJIMENTI |
|---|---|---|
| Kilimo cha mikorosho, ufuta, matunda, miboga, viazi vitamu, mtama, mpunga, muhogo na ndizzi. | Kinafanyika zaidi katika uwanda wa mafuriko (kaskazini na Kusini kwa Mto Rufiji kati ya Mloka mpaka Ikwiriri). Katika Delta hufanyika Chumbi na Mbwara. | ➢ Uharibifu wa mazao ya wanyama pori kama vile tembo, viboko, nguruwe mwitu, nyani,<br>➢ Ukame,<br>➢ Bei duni kwa mapato ya mazao,<br>➢ Zana hafifu za kilimo,<br>➢ Soko duni kwa mazao yao kama matunda, na<br>➢ Mafuriko,<br>➢ Huduma duni za upanuzi,<br>➢ Ukosefu wa zana za kilimo za kisasa |
| Nazi, mpunga | Ukanda wa Pwani, Uwanda wa Mafuriko wa Rufiji (kwa mpunga) | ➢ Mfumo duni wa usafiri(maji na ardhi) na hivyo upatikanaji mdogo wa masoko,<br>➢ Bei duni za bidhaa,<br>➢ Migogoro kati ya wakulima na mameneja wa rasilimali za mikoko juu ya upandaji mpunga katika delta,<br>➢ Matatizo ya mipaka ya vijiji,<br>➢ Uharibifu wa sehemu zenye mvua nyingi unaosababishwa na usafishaji kwa ajili ya kilimo cha mpunga,<br>➢ Uchafuzi wa Mazingira kama matokeo ya kutumia kemikali kuulia kaa wala mpunga- matumizi ya dawa ya kuulia wadudu (DDT) umeshuhudiwa katika Delta,<br>➢ Huduma duni za upanuzi,<br>➢ Ukosefu wa aina mbalimbali za mpunga unaotoa mazao mengi unaosababisha uanzishaji wa maeneo mapya ili kuboresha uzalishaji. |
| Ufugaji wa mifugo | Kilimani, Mkongo, Ikwiriri, Mohoro,Utete, Mbwera na Kusini mwa delta | ➢ Ufugaji duni wa mifugo,<br>➢ Kipato duni kitokanacho na mifugo |
| Maji kwa matumizi ua nyumbani, umwagiliaji, | Mbunju (Segeni), Mkongo<br>Uwanda wa mafuriko na delta ya Rufiji | ➢ Mashambulizi toka kwa mamba(mapambano ya binadamu na wanyamapori),<br>➢ Kujipenyeza kwa maji ya chumvi katika maji safi ya visima, |

| SHUGHULI | ENEO | MASUALA YA MENEJIMENTI |
|---|---|---|
| usafiri | | ➢ Nyenzo za usafiri, zisizoaminika mf. Mitumbwi<br>➢ Mafuriko ya mara kwa mara,<br>➢ Ukosefu wa maji ya kunywa salama |
| Utafutaji Mafuta | Bonde la mto Rufiji toka Kisangire hadi Mtunda | ➢ Kuondoa mimea (ya asili ya kuliwa) kwa ajili ya njia za tetemeko,<br>➢ Njia za tetemeko na barabara zilizoboreshwa zikiwa zinatumika na majangili na wakataji magogo kusafirishia shehena zao nje ya wilaya |
| Bomba la gesi | Eneo kwa bomba la gesi toka Somanga, Mohoro, mpaka Ndundu | ➢ Kuondoa mimea,<br>➢ Mabomba yanayoelekea kupasuka ambayo yangeweza kuharibu mfumo wa ikolojia tokana na kuvuja kwa gesi |
| Utoaji chumvi | Delta ya Rufiji | ➢ Kukata mikoko ili kukausha maji ya bahari,<br>➢ Mapato duni ya uchumi |

## 5.2 Kikundi cha Wanyama Pori

| SHUGHULI | ENEO | MASUALA YA MENEJIMENTI |
|---|---|---|
| Ujangili wa wanyama katika Hifadhi ya Wanyama ya Selous na maeneo mengine ya mbuga yaliyo wazi . | Vijiji vyote vinavyozunguka Hifadhi ya Mbuga ya Selous na maeneo ya wazi ya Mohoro,Ngukukula, na Mkongo | ➢ Ujangili wa wanyama pori,<br>➢ Kuenea kwa moto wa misitu |
| Mapambano kati ya binadamu na wanyamapori | Imeenea kwa mapana katika eneo la mradi | ➢ Maofisa wa wanyamapori wasiotosheleza toka Halmashauri ya wilaya ya Rifiji kufuatilia na kukomesha wanyama waharibifu,<br>➢ Vifaa visivyotosheleza kwa wafanyakazi wa wilaya na wakazi wenyeji wa kijiji kuzuia uharibifu,<br>➢ Wilaya zilizopo hazihamasishwi kutekeleza kazi zao,<br>➢ Upanuzi wa shughuli za kilimo kwenye maeneo wazi ya wanyam pori,<br>➢ Upanuzi wa hifadhi ya wanyama pori kwa maeneo ya kilimo ,<br>➢ Mifumo jamii ya asili kwa ajili kuyamudu matatizo inavunjwa. |
| Uwindaji | Maeneo ya wazi hasa vijiji vya Tapika, Ngarambe na Mloka | ➢ Idadi ya kikomo haikuzingatia idadi halisi ya wanyama pori kwani sensa ya wanyama ilifanyika kabla,<br>➢ Ukosefu wa taarifa za mara moja katika kila msimu,<br>➢ Wengi wa wawindaji wanatoka nje ya wilaya ya Rufiji, kwa hiyo wengi wa wenyeji wa wilayani hawanufaiki na shughuli za uwindaji,<br>➢ Wanakijiji wanaowinda hupata mapato ya chini ukilinganisha na kile ambacho wangepata iwapo wangefanya biashara ya uwindaji wa halali,<br>➢ Uwindaji haramu kwa nyama pori,<br>➢ Ofisi ya wanyama pori ya wilaya ina wafanyakazi wachache hivyo kufanya ufuatiliaji wa shughuli za uwindaji kuwa mgumu,<br>➢ Uwindaji kwa kutumia njia haramu kama vile mitego na |

| SHUGHULI | ENEO | MASUALA YA MENEJIMENTI |
|---|---|---|
| | | kuwapiga kwa shoka hadi kufa,<br>➢ Ufahamu mdogo na ukosefu wa taarifa kuhusu sera na sheria za menejimenti ya maliasili,<br>➢ Maafisa wanyamapori wakati mwingine hawafuati kanuni zilizowekwa kuhusu uwindaji. |
| Utalii | Hasa katika Hifadhi ya Mbuga ya Selous, lakini pia shughuli chache za utalii katika vijiji vinavyoizunguka kama Mloka, Tapika na pia katika Delta | ➢ Utalii ambao ni muhimu katika wilaya ya Rufiji haujaendelezwa kikamilifu,<br>➢ Maarifa na ufahamu mdogo kuhusu utalii unategemea jamii, katika ngazi yoyote ya wilaya,<br>➢ Wawekezaji kutokubali kuendeleza shughuli za utalii katika wilaya ya Rufiji,<br>➢ Uwezekano wa kutokuelewana kuhusu umiliki katika eneo la kaskazini ya Ziwa Utunge,<br>➢ Shinikizo lililoongezeka katika maeneo yanayopatikana na HMS yanategemewa kwani hifadhi hiyo inazuia maendeleo zaidi ya utalii katika mbuga hiyo,<br>➢ Uvumbuzi wa mafuta katika delta ya kona ya kaskazini Magharibi ya Wilaya ya Rufiji ingeweza kutishia utalii/kupunguza thamani kwa utalii. |

## 5.3 Kikundi cha Rasilimali ya Misitu

| SHUGHULI | ENEO | MASUALA YA MENEJIMENTI |
|---|---|---|
